



ظلم کا انجام

MATOKEO YA DHULMA

(SWAHILI)



Shaikh-e-Taariqat Ameer-e-AhleSunnat
Mwanzilishi wa Dawat-e-Islami,
Allama Moullana Abu Bilal

MUHAMMAD ILYAS

Attar Qadiri Razavi

کاتب القرآن
المستجاب



ظلم کا انجام

MATOKEO YA DHULMA

Kitabu hiki kimeandikwa na Sheikh-e-Tarīqat Amīr-e-Ahl-e-Sunnat, muasisi wa Dawat-e-Islami ‘Allāmah Maulānā Abu Bilal Muhammad Ilyas ‘Attar Qadiri Razavi داعوتِ برکاتِہو العالیہ kwa **kiUrdu**. Kikatafsiriwa na Majlis Tarajim kwa **Kiswahili**. Ikiwa utakipata na makosa yoyote, tafadhali wajulishe Majlis kwa kutumia anwani ya posta au kipepesi kifuatacho kwa nia ya kupata thawabu.

Majlis ya Kutafsiri ya Dawat-e-Islami

Alami Madani Markaz, Faizan-e-Madinah, Mahallah
Saudagran, Purani Sabzi Mandi, Bab-ul-Madinah,
Karachi, Pakistan

Mawasiliano: ☎ +92-21-34921389 to 91

Barua pepe: ✉ translation@dawateislami.net

الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ وَالصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ عَلَى سَيِّدِ الْمُرْسَلِينَ
أَمَّا بَعْدُ فَأَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Du'a Kabla ya Kusoma Kitabu

Soma dua ifuatayo kabla ya kusoma kitabu au somo la kidini.
إِنْ شَاءَ اللَّهُ عَزَّوَجَلَّ utakumbuka yote uliyoyasoma.

اللَّهُمَّ افْتَحْ عَلَيْنَا حِكْمَتَكَ وَأَنْشُرْ
عَلَيْنَا رَحْمَتَكَ يَا ذَا الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ

Tafsiri

Ee Mola عَزَّوَجَلَّ ifungue milango ya elimu na busara kwa ajili yetu, na utuhurumie! Ewe uliye Mtakatifu kabisa.

(Al-Mustafraf, juz. I, uk. 40, Dar-ul-Fikr, Beirut)

Kumbuka: Mswalie Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ mara moja kabla na baada ya dua.

Transliteration Chart

ء	A/a	ژ	Ř/ř	ل	L/l
ا	A/a	ز	Z/z	م	M/m
ب	B/b	ژ	X/x	ن	N/n
پ	P/p	س	S/s	و	V/v,
ت	T/t	ش	Sh/sh		W/w
ٹ	Ṭ/ṭ	ص	Ṣ/ṣ	ه / ه / ة	Ĥ/ĥ
ث	Ṣ/ṣ	ض	Ḍ/ḍ	ی	Y/y
ج	J/j	ط	Ṭ/ṭ	ے*	Y/y
چ	Ch	ظ	Ẓ/ẓ	ـ	A/a
ح	H/h	ع	‘	ُ	U/u
خ	Kh/kh	غ	Gh/gh	ـ	I/i
د	D/d	ف	F/f	و مدّه	Ū/ū
ڈ	Ḍ/ḍ	ق	Q/q	ی مدّه	Ī/ī
ذ	Ẓ/ẓ	ک	K/k	ا مدّه	Ā/ā
ر	R/r	گ	G/g		

Yaliomo

Du'a Kabla ya Kusoma Kitabu	ii
Transliteration Chart	iii

MATOKEO YA DHULMA 1

Taji la lulu	1
Jambazi katili.....	2
Madhalimu hucheleweshewa adhabu yao.....	3
Kutupwa kichwa kichwa Motoni	4
Pingu za moto	4
Nani Muflisi?.....	5
Mtu anafaa aogope.....	6
Tufaha nusu.....	7
Balaa kwa kuchokoa meno kwa kijiti.....	7
Madhara ahera kwa kutunda tembe ya ngano.....	8
Sala mia saba za jamaa	9
Hairuhusiwi kuchelewesha kulipa deni bila sababu.....	10
Ustaarabu katika kulipa deni.....	11
Tajiri wa matendo mema.....	11
Anayemuudhi Allah ﷺ na Mtume wake ﷺ.....	12
Muwasho wa ajabu.....	13
Kustarehe Peponi	14

Matokeo ya Dhulma

Unyenyekevu wa ajabu wa Mtume Mtukufu ﷺ	14
Nimekusongonyoa sikio.....	15
Muislamu ni nani?.....	15
Kupiga Muislamu jicho na kumtisha	16
Tuwapole kwa wapole na.....	16
Hata dhalimu usimdhulumu.....	17
Safari ya kurudisha kalamu ya mwenyewe.....	18
Vipi unavaa slipa za mwenyewe bila ruhusa?	18
Alivyokuwa na tahadhari kwa kuvuta harufu ya manukato.....	19
Kuzima kandili!.....	20
Bustani la Peponi au Shimo la Motoni.....	20
Tende nusu.....	21
Matokeo ya kofi la mfalme	21
Sayyidunā ‘Umar al-Fārūq aliishi maisha ya Kawaida ﷺ	22
Sababu za mwisho mbaya.....	23
Je, ni vipi kujiita mtumwa wa mwengine?	24
Wasikiaje?	24
Ufafanuzi wa ‘Nitaonekana mnafiki’	25
Ni muhimu kumsaidia madhulumu	25
Miale ya moto ilikuwa inatoka kaburini	26
Huruma kwa waislamu.....	26
Huruma kwa mwizi.....	27

Adhabu ya ujambazi	27
Mau ya Madani kwa wale wanaowatibu waovu	28
Mbinu za kujifunza haki za wengine	28
Namna mbalimbali za kudhulumu	29
Ni dhambi kumfanyia mtu mzaha	30
Adhabu kwa kukejeli wengine	30
Tafadhali omba msamaha	31
Nimeshamsamehe.....	32
Pesa zirudishwe	33
Namna ya kuomba msamaha wale tuliowasahau	34
Allah ﷻ atapanga kupatana	34
Maua 12 ya Madani yanayohusu mazungumzo	36

الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ وَالصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ عَلَى سَيِّدِ الْمُرْسَلِينَ
أَمَّا بَعْدُ فَأَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

MATOKEO YA DHULMA*

Ingawa Shetani hatojali kufanya bidii ili kukutiya uvivu, kisome kijitabu hiki chote; **إِنْ شَاءَ اللَّهُ عَزَّوَجَلَّ**, utamalizikia kutiririkwa na machozi kwa kumcha Allah **عَزَّوَجَلَّ**.

Taji la lulu

Imeelezwa katika *Al-Qaul-ul-Badī'*, kuwa baada ya kifo cha Sayyidinā Sheikh Aḥmad bin Manṣūr **عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْعَظِيمَا**, mtu mmoja alimuota amesimama kwenye miḥirabu ya msikiti wa Jamia ulioko Shirāz akiwa amevaa joho la Peponi na taji la lulu kichwani. Aliyeota akauliza, **‘مَا فَعَلَ اللَّهُ بِكَ؟’**: “Alikutendea nini Allah **عَزَّوَجَلَّ**?” Akajibu, “Allah **عَزَّوَجَلَّ** amenisamehe, amenikirimu na kunivalisha taji la lulu na akaniingiza Peponi.” Akauliza zaidi, “Na zawadi hii ni ya nini?” Sheikh Aḥmad bin Manṣūr **عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْعَظِيمَا** akajibu,

* Amir Ahl-e-Sunnat alitoa bayana hii katika hafla ya siku 3 ya Sunna ya Dawat-e-Islami, Shirika la Kueneza Mafundisho ya Qur'an na Sunna Lisilojihusisha na Siasa, Sahra-e-Madinah Multan mwaka wa 1429 AH (2008 AD). Kimechapishwa kikiwa na mabadiliko machache.

‘الْحَمْدُ لِلَّهِ عَزَّوَجَلَّ’ Nilikuwa nikimswalia kwa wingi Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ; hii ndiyo amali iliyonifaidisha mimi.” (*Al-Qaul-ul-Badi’*, uk. 254)

Jambazi katili

Sheikh ‘Abdullāh Shāfi’ī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللهِ الْقَوِي ameeleza katika safari zake: “Siku moja tulitoka Basrah kuelekea kijijini. Karibu na wakati wa Alasiri, tulivamiwa ghafla na jambazi katili. Jambazi alimua mwenzangu. Baada ya kunipokonya pesa na vitu vyangu; alinifunga kamba, akanibwaga chini na akatoroka. Kwa namna fulani, niliweza kujifunga na nikaendelea na safari lakini kwa sababu ya hofu niliyokuwa nayo, nilisahau njia mpaka jua likatwa. Nikaelekea upande nilioona moto ukiwaka. Baada ya hatua chache nikaona hema, kwa sababu ya kuchoka na kiu kali, nilisimama mlangoni, nikaita: **الْعَطَشُ! الْعَطَشُ!** “Jamani kiu! Jamani kiu!” Kwa bahati mbaya, hema lilikuwa la yule jambazi katili. Badala ya kuniletea maji, jambazi alitoka na upanga kwa nia ya kunivamia na kunimaliza mara moja. Mkewe alijaribu kumzuia lakini hakumsikiliza. aliniburuta hadi msituni, akanikalia kifuani, akauweka upanga wake shingoni mwangu karibu kunichinja, mara akatokea simba vichakani. Jambazi alipomuona simba, akaanguka kwa uoga. Simba alimvamia na kumraruarua vibaya halafu akapotelea vichakani. Nilimshukuru Allah عَزَّوَجَلَّ kwa uokozi wake.

Madhalimu hucheleweshewa adhabu yao

Ndugu waislamu wapenzi! Je, mumetanabahi matokeo mabaya ya udhalimu? Sayyidunā Sheikh Muhammad bin Ismā'il Bukhārī عَلِيهِ رَحْمَةُ الْبَارِي ametaja katika 'Ṣaḥīḥ al-Bukhārī': Sayyidunā Abū Mūsā Ash'arī رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ amesema kwamba Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema, “Hakika, Allah عَزَّوَجَلَّ humcheleweshea dhalimu adhabu, hadi siku atakapomshika, hatomuacha tena.” Baada ya kusema haya, Mtukufu Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alisoma Sūrah̄ Hūd (Sūra ya 11) aya ya 102:

وَكَذَلِكَ أَخْذُ رَبِّكَ إِذَا أَخَذَ الْقُرْآنَ وَهِيَ ظَالِمَةٌ إِنَّ أَخْذَهُ أَلِيمٌ شَدِيدٌ ﴿١٠٢﴾

Na ndiyo kama hivyo ndivyo inavyokuwa Mola wako Mlezi anapoikamata miji inapokuwa imedhulumu, hakika mkamato wake ni mchungu na makali.

[Kanz-ul-Īmān (Translation of Quran)] (Sūra 12, Sūrah̄ Hūd, Aya 102;

Ṣaḥīḥ Bukhārī, juzuu 3, uk. 247, Hadithi 4686)

Magaidi, majambazi, wauaji na wahalifu wazingatie visa hivyo vilivyoelezwa. Wasisahau matokeo ya uovu wao kwani inapowateremkia na ghadhabu ya Allah عَزَّوَجَلَّ, hufa ki-mbwa. Na hakuna wa kuwahurumia. Zaidi ya hayo, kutakuwa na adhabu kali ahera ambayo hakuna atakayeweza kuivumilia. Ni wazi kwamba kugandamiza watu ni dhambi. Huleta madhara duniani na ahera na kusababisha adhabu ya Motoni. Udhalimu ni kwenda kinyume na maamrisha ya Allah عَزَّوَجَلَّ na Kipenzi chake Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ na pia ni kuvunja kanuni za haki za kibinadamu.

Sheikh Jurjānī عَدَسٌ بَيْرُتُ الدُّرَابِي ametoa maelezo ya udhalimu katika kitabu chake, التَّعْرِيفَات: “Ni matumizi mabaya ya kitu.” (*At-Ta’rīfāt-lil-Jurjānī, uk. 102*) Katika sharia, dhuluma ni kumnyang’anya mtu haki yake au kukitumia kitu vibaya au kuadhibu mtu bila sababu.” (*Mirāt, juzuu. 6, uk. 669*)

Jambazi ambaye umesoma kisa chake, alikuwa akiwaua watu wasiokuwa na hatia, akiwaibia na kuwanyang’anya; aliona adhabu yake hapa hapa duniani, na hakuna ajuaye adhabu atakayopata kaburini mwake. Zaidi ya hayo hesabu yake ya Siku ya Kiama bado hijafanyika. Hata leo, ni kawaida wevi, wanyang’anyi hawachelei kuua watu. Kumbuka ni dhambi kubwa kuua bila sababu!

Kutupwa kichwa kichwa Motoni

Sayyidunā Muhammad bin ‘Īsā Tirmizī عَلِيٌّ مُحَمَّدٌ اللَّهِ الْقَوِي, katika mkusanyo wake maarufu wa Hadithi ‘*Tirmidhī*’, ameeleza kutoka kwa Sayyidunā Abū Sa’īd Khudrī na Sayyidunā Abū Ḥurāirah رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهُمَا, “Ikiwa viumbe vyote vilivyoko mbinguni na ardhini wakishiriki kumuua Muislamu mmoja, Allah عَزَّ وَجَلَّ atawatupa wote Motoni kichwa kichwa.” (*Sunan Tirmidhī, juzuu. 3, uk. 100, Hadīthi 1403*)

Pingu za moto

Wanaowalaghai watu pesa zao, wanaovunja majumba na kuiba, wanaodai pesa kwa kutuma barua za vitisho, wazingatiye. Leo mali ya haramu inaonekana nyepesi kuteremsha tumboni lakini

kesho Siku ya Kiama, inaweza kuleta matatizo makubwa. Enyi watu sikizeni! Sayyidunā Faqīh Abul Laiš Samarqandī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْقَوِيّ ameeleza katika ‘Qurra-tul-‘Uyūn’: Hakika, kuna pingu za moto katika kivuko cha Şirāṭ. Aliyechukuwa hata shilingi moja kwa njia za haramu; miguu yake itafungwa kwa pingu za moto. Pingu hizi zitamtatiza kuvuka kivuko cha Şirāṭ mpaka mwenye shilingi alipwe malipo yake kutoka kwa matendo yake mema. Na ikiwa matendo yake mema yatamalizika, basi atabeba mzigo wa dhambi za mwenye shilingi; matokeo yake ni kuingia Motoni. (*Qurra-tul-‘Uyūn ma’ Al-Rauḍ al-Fāṭiq, uk. 392*)

Nani Muflisi?

Sayyidinā Muslim bin Ḥajjāj Qushayrī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْقَوِيّ ameeleza katika mkusanyiko wake mashuhuri wa Ḥadīthi ‘*Ṣaḥīḥ Muslim*’: Mtume Kipenzi صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ aliuliza, ‘Je, munamjua muflisi? Maswahaba waliobarikiwa عَلَيْهِمُ الرِّضْوَانُ wakajibu, “Yā Rasūlullāh صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ, tunavyomjua sisi muflisi ni yule ambaye kati yetu hana mapeni wala rasilimali nyengine.” Mtume kipenzi صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akajibu, “Katika umma wangu, muflisi ni yule ambaye atakuwa na salā, saumu na zaka Siku ya Kiama lakini atakuwa ametukana au amemnyang’nganya mtu pesa, ameuwa, amepiga mtu; kwa hivyo matendo yake mazuri yatachukuliwa kulipa aliwoadhulumu; ikiwa, matendo yake mazuri yote yatamalizika kabla hajamaliza kulipa aliwoadhulumu basi madhambi ya wadhulumiwa yatahamishwa kwake na halafu atatupwa Motoni.” (*Ṣaḥīḥ Muslim, uk. 1394, Ḥadīthi 2581*)

Mtu anafaa aogope...

Enyi munaosimamisha sala, Enyi munaofunga mwezi wa Ramadhani, Enyi munaofanya Hajj, Enyi munaotoa zaka ipasavyo, Enyi munaotoa sadaka, Enyi matajiri wenye sura za watu wema, ogopeni na mutetemeke! Hakika muflisi ni yule ambaye ingawa amefanya matendo mema kama vile sala, kufunga, kutoa zaka, kwenda hajj, kutoa sadaka na huduma za kusaidia jamii; atabakia mtupu bila chochote Siku ya Kiama. Kwa Yule ambaye wakati mwengine ameuadhi watu kwa kuwatusi au kuwaadhibu kwa njia ambayo sheria hairuhusu au kupiga au kusudi kutoregesha vitu alivyoazima, au kutolipa deni au kuudhi watu; watu kama hao watasomba amali zake nzuri zote na zikimalizika atabeba mzigo wao wa dhambi na atatupwa katika Moto wa Jahanamu.

Imeelezwa katika ‘*Ṣaḥīḥ Muslim*’ kwamba Mtume Kipenzi صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema, “Enyi watu, itawabidi muregeshe haki za wenye haki, hata mbuzi mwenye pembe atalipwa kwa mbuzi asiyekuwa na pembe.” (*Ṣaḥīḥ Muslim, uk. 1394, Hadithi 2582*)

Ina maana kuwa ikiwa hukutimiza haki za watu katika dunia hii, basi utalipa haki zao Siku ya Kiama- duniani utalipa kwa pesa na katika maisha ya ahera kwa matendo yako mazuri. Kwa hivyo ni vyema kuheshimu haki katika maisha ya duniani ili kuepuka majuto ya ahera.

Imetajwa katika *Mirāt Sharḥ Mishkāt*, “Ingawa wanyama hawana hukumu katika sheria, lazima watalipa haki kwa viumbe wenzao.”

(Mirāt, juzuu. 6, uk. 674)

Wale wanaomcha Allah ﷻ katika upande wa kuchunga haki za binadamu, hata katika mambo yasiyokuwa na uzito, wanakuwa waangalifu kwa kiasi ambacho hutuacha na mshangao.

Tufaha nusu

Sayyidinā Ibrāhīm bin Adḥam رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى alipata tufaha ndani ya mkondo wa maji. Aliliokota na kulila lote. Baada ya kula tu, alijuta kufanya hivyo. Yaani kulila bila ya ruhusa ya mwenyewe! Kwa hivyo alielekea shambani kumtafuta mwenyewe. Akapata mwanamke kuwa ndiye aliyekuwa mwenye shamba. Akaomba msamaha kwa tendo lake. Mwanamke akasema, “Shamba hili ni letu, mimi na mfalme; nimekubali msamaha wako kutokana na haki yangu lakini sina idhini ya kukusamehe kwa niaba ya mfalme.” Mfalme alikuwa yuko Balkh, kwa hivyo Ibrāhīm bin Adḥam رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى akafunga safari kuelekea huko na hakutulia mpaka alipofaulu kuupata msamaha kutoka kwa mfalme. *(Raḥlah*

Ibn-e-Baḥūṭāh, juzuu 1, uk. 34)

Balaa kwa kuchokoa meno kwa kijiti

Ndugu wapenzi waislamu! Kuna mafunzo mengi katika kisa hicho kwa wale ambao hudhulumu wengine na kunyakuwa bidhaa madukani bila kulipa. (mfano matunda, mboga na kadhalika) Iwapo watahukumiwa Siku ya Kiama kwa matendo kama hayo

wanayoyaona kuwa ni ya kawaida, watafanya nini? ‘Allāmah ‘Abdul Wahhāb Sha’rānī عبد الوهاب بن محمد بن عبد الوهاب ameeleza katika ‘*Tanbīh-ul-Mughtarīn*’: Mwanachuoni maarufu Sheikh Sayyidunā Wahhāb bin Munabbih رحمته الله تعالى عنه amesema: Mtu mmoja katika banuu Israili alitubia madhambi yake yote ya awali, halafu akafanya ibada kwa miaka sabini mfululizo kwa kufunga mchana na kusimama usiku akifanya ibada; hakula chakula kitamu wala kupumzika chini ya kivuli. Baada ya kufa, mtu mmoja alimuota na akamuuliza ‘مَا فَعَلَ اللَّهُ بِكَ؟’ “Allah عَزَّوَجَلَّ amekuhukumu vipi?” Akajibu, “Allah عَزَّوَجَلَّ alinihakumu kwa matendo yangu, akanisamehe dhambi zangu zote ila kwa kipande cha mti nilichookota ambacho nilitumia kuchokoa meno bila ya ruhusa ya mwenyewe na sikuweza kumuomba msamaha kwa hivyo nimezuiwa kuingia Peponi (kwa sababu linahusiana na haki ya binadamu) (*Tanbīh-ul-Mughtarīn*, uk. 51)

Madhara ahera kwa kutunda tembe ya ngano

Ndugu waislamu wapenzi! Tafadhali tafakarini juu ya kipande cha mti kilichomzuia mtu kuingia Peponi. Kuchokoa meno kwa kipande cha mti kisicho na thamani yaonekana ni jambo dogo ikilinganishwa na watu ambao siku hizi huibia wenzao mamilioni na mabilioni. Allah عَزَّوَجَلَّ atuongoze katika njia ya haki! آمين

Sikilizeni kisa kingine chenye mazingatio kinachohusiano na kuangamia kwa mtu Siku ya Kiama kwa ajili ya kutunda tembe ya ngano (siyo kula) bila ya ruhusa ya mwenyewe. Inaelezwa kwamba mtu mmoja alimuota mtu aliyekufa na akamuuliza:

“مَا فَعَلَ اللَّهُ بِكَ؟” Allah عَزَّوَجَلَّ amekuhukumu vipi?” Akajibu, “Allah عَزَّوَجَلَّ amenisamehe lakini hesabu yangu imefanywa na nikaulizwa siku ambayo nilikaa katika duka la rafiki yangu nikiwa katika saumu. Ilipofika wakati wa kufungua, nilichukua tembe ya ngano nikaikuvunja na nikataka kuitia mdomoni; nilipotanabahi kuwa haikuwa yangu nikairegesha. Kwa hivyo nilihukumiwa kwa kuchukua tembe ya ngano ya mtu mwengine na amali yangu njema ikapunguzwa kwa kiwango sawa na hasara niliyoisababisha ya kuivunja.” (*Mirqāt-ul-Mafāih, juzuu 8, uk. 811, Tahat-al-Hadithi 5083*)

Sala mia saba za jamaa

Ndugu wapenzi waislamu! Je, mumegundua kuwa hata kutunda tembe ya ngano ya mwenzako kunaweza kukuletea hasara ahera! Nani anayezingatia kutunda au kula tembe ya ngano, ilihali siku hizi watu hula chakula kamili kwa kuvamia sherehe za wenyewe bila kualikwa ingawa sheria hairuhusu. Imeelezwa katika hadithi ya Abū Dāwūd: “Anayehudhuria sherehe bila kualikwa, ameingia akiwa ni mwizi na ametoka akiwa ameshapora.” (*Sunan Abī Dāwūd, juzuu. 3, uk. 379, Hadithi 3741*)

Zaidi ya hayo watu siku hizi huwapora watu maelfu au hata mamilioni kwa jina la mkopo. Katika maisha ya dunia, yaonekana ni jambo rahisi na la kuvutia lakini litakuwa ni jambo zito Siku ya Kiama. Enyi ambao hamumalizi kulipa madeni ya watu sikizeni kwa makini! Imām Aḥmad Razā Khān رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَلَيْهِ ameeleza, “Yule ambaye hatamaliza kulipa madeni hata kama ni

senti tatu, itambidi atoe sala mia saba za jamaa kama fidia Siku ya Kiama.” (*Fatāwā Razawīyyah, juzuu. 25, uk. 69*)

Inaeleweka kuwa anayempora mwenzake pesa ni mnyama na hakika anajidhuru yeye mwenyewe. Katika mkusanyo wa hadithi zake ‘*Ṭabarānī*,’ Sayyidinā Sulaymān Ṭabarānī مُحَمَّدُ بْنُ سُوْدَةَ التُّورَانِي ametaja riwaya hiyo ya Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ: “Matendo mema ya mgandamizaji atapewa mgandamizwaji, na dhambi za mgandamizwaji atapewa mgandamizaji.” (*Al-Mu’jam-ul-Kabīr, juzuu. 4, uk. 148, Ḥadīthi 3969*)

Hairuhusiwi kuchelewesha kulipa deni bila sababu

Hebu niwapatie habari muhimu kuhusu deni. Sayyidinā Imām Muhammad bin Muhammad Ghazālī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللهِ الْوَالِي ameeleza katika *Kīmīyā-e-Sa’ādat*, “Anayechukua mkopo na anuie kuwa atalilipa kikweli, Allah عَزَّوَجَلَّ huchaguwa malaika wanaomuhifadhi na kumuombea deni lilipwe.” (*Tazama: Itḥāf-us-Sādah-liz-Zubaydī, juzuu. 6, uk. 409*)

Ikiwa aliyechukua deni ana uwezo wa kulipa na acheleweshe kulipa bila ya kuelewana na mkopaji, basi kuchelewesha hata kama ni kidogo ni dhambi na mdeni atachukuliwa kuwa muovu na mgandamizaji awe yuko katika saumu au kulala, dhambi zitaendelea kuandikwa katika hesabu yake. Na kila wakati atakuwa katika laana ya Allah عَزَّوَجَلَّ. Hii ni dhambi ambayo hata ukilala unabakia nayo. Ikiwa anaweza kulipa deni kwa kuuza mali yake, inambidi afanye hivyo au sivyo atakuwa mtenda dhambi. Ikiwa

katika kufidia deni atalipa kwa kitu ambacho hakikumridhisha mkopeshaji, basi atahesabiwa kuwa mtenda dhambi mpaka amridhishe; kwa sababu tendo lake hili linahesabiwa kuwa dhambi kubwa. Lakini watu hawazingatii jambo hili. (*Kīmīyā-e-Sa'ādat, juzuu. 1, uk. 336*)

Ustaarabu katika kulipa deni

Ndugu waislamu! Watu wanapokuwa wahitaji huwa na maneno matamu kwa mkopeshaji ili awakopeshe. Lakini wanapopata, hawasghughuliki hata kulipa. Ustaarabu ni kumwendea nyumbani na kumlipa pamoja na kumshukuru. Lakini linalofanyika leo, ikiwa basi deni litalipwa, kwanza ni kumuudhi mkopeshaji kwa kuchelewesha kumlipa na kumregesha mara kwa mara anapokuja kudai, pili pesa hulipwa kidogo kidogo badala ya zote. Kumbuka! Kumuudhi mkopeshaji bila sababu muhimu ni udhalimu. Kawaida, wafanyabiashara wanatabia ya kuahirisha kumlipa mkopeshaji kwa kumwambia “Njoo jioni au kesho au baada ya siku kadhaa.” Bila sababu ya sharia na huwakatisha tamaa wakopeshaji ilihali pesa wanazo. Hawajali kuwa wanajiletea madhara makubwa. Ikiwa unapesa na unapanga kuzilipa jioni, ni jambo gani linalokuzia kulipa mapema asubuhi?

Tajiri wa matendo mema

Ndugu waislamu! Uvunjaji haki za binadamu ni kosa kubwa kwa maisha ya ahera. Sayyidinā Aḥmad bin Ḥarb رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ amesema, “Watu wengi watakufa wakiwa matajiri wa amali njema lakini

kwa ajili ya kuvunja haki za binadamu, watapoteza amali zao Siku ya Kiama hivyo basi watakuwa masikini na mafukara.” (*Tanbīh-ul-Mughtarīn*, uk. 53)

Sayyidinā Abū Tālib Muhammad bin ‘Alī Makkī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْقَوِيّ amesema katika ‘*Qūt-ul-Qulūb*’, “Mara nyingi, watu watarushwa Motoni kwa sababu ya madhambi ya wengine, (wala si kwa madhambi yao) Vile vile, watu wengi wataingia peponi (si kwa amali zao njema), bali kwa kupata amali njema kutoka kwa wengine.” (*Qūt-ul-Qulūb*, juzuu. 2, uk. 292)

Ni wazi kuwa wale ambao wameudhiwa na haki zao kubatilishwa duniani, watapata amali njema za wengine. Kwa hivyo waliogandamizwa na walioteswa watafaidika Siku ya Kiama.

Anayemuudhi Allah ﷺ na Mtume wake ﷺ

Swala la haki za binadamu ni nyeti mno, lakini leo mbali na watu wa kawaida na hata wasomi hawalitili maanani. Hasira ni ugonjwa ulioenea. Hasira hii huwafanya hata watu wasomi kuwadhi wengine na hawatanabahi kuwa kuudhi wengine pale ambapo sharia hairuhusu ni haramu na ni sababu ya kumpeleka Motoni. Imām Aḥmad Razā Khān عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى ameeleza katika *Fatāwā-e-Razawīyyah*, juzuu 24, ukurasa 342, kwa kumrejelea Ṭabarānī: Mtume Mtukufu صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema: ‘مَنْ أَدَى مُسْلِمًا فَقَدْ أَدَانِي‘، ‘وَمَنْ أَدَانِي فَقَدْ أَدَى اللَّهَ’، “Mwenye kumuudhi muislamu ameniudhi mimi, na mwenye kuniudhi mimi, amemuudhi Allah ﷺ. (*Al-Mu’jam-ul-Awsaṭ*, juzuu. 2, uk. 387, *Hadithi 3607*)

Allah ﷺ amesema katika sura ya 22, Sūrah Ahzāb, aya 57, kuhusu wale wanaomuudhi Allah ﷺ na Mtume wake Kipenzi صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ:

إِنَّ الَّذِينَ يُؤْذُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ لَعَنَهُمُ اللَّهُ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ
وَأَعَدَّ لَهُمْ عَذَابًا مُهِينًا ﴿٥٧﴾

Hakika wale wanaomuudhi Allah na Mtume wake Mtukufu – juu yao ni laana ya Allah duniani na ahera na Allah amewatayarishia adhabu ya kufedehesha.

[Kanz-ul-Īmān (Translation of Quran)] (Sūra 22, Sūrah Ahzāb, Aya 102)

Muwasho wa ajabu

Ndugu waislamu! IKiwa umemuudhi mtu, iwapo ni kaka yako, babako, mke wako, mkwe wako, hata raisi, waziri mkuu, mwalimu, kiongozi wa dini, muadhini, au imamu na khatibu, tubia kwa Allah ﷺ bila kuchelewa, halafu muombe msamaha uliyemuudhi na umshawishi mpaka aridhike kwani haivumiliki adhabu kali ya Motoni.

Sikiza kwa makini, Sayyidinā Yazīd bin Shajarāh رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ amesema, “Moto unamipaka kama ufuo wa bahari, unakaliwa na nyoka mfano wa ngamia wanaokwenda kasi na nge mfano wa nyumbu. Wakati watu wa Motoni watakapoomba kupunguziwa adhabu, wataambiwa watoke kupitia mipakani. Watakapotaka kutoka, nyoka watawashika midomo na nyuso zao na kurarua

ngozi zao. Watakimbilia motoni ili wajiokowe. Halafu wataadhibiwa kwa ugonjwa utakao sababisha muwasho wa ajabu. Watajikuna mno mpaka ngozi yao itabambuka na kubakisha mifupa tu, halafu itatangazwa: “Ewe fulani wa fulani, unasikia maumivu?” ataitikia, “Ndiyo”. Halafu ataambiwa: “Haya ni malipo ya maudhi ambayo ulikuwa ukiwafanyia waislamu.” (*Attarghīb Wattarhīb, juzuu. 4, uk. 280, Hadithi 5649*)

Kustarehe Peponi

Ndugu waislamu! Muislamu hamuudhi muislamu mwengine; badala yake jukumu lake ni kuwakinga waislamu kudhuriwa na chochote. Sayyidinā Imām Muslim bin Ḥajjāj Qushayrī رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ alieleza katika Saḥīḥ Muslim ya kwamba Mtume kipeenzi صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ katika hadithi sahihi amesema, “Nilimuona mtu akitembea peponi, na alikuwa akienda popote alipotaka kwa sababu alipokuwa duniani alikata mti uliokuwa ukiwaudhi watu njiani.” (*Saḥīḥ Muslim, uk. 1410, Hadihi 2617*)

Unyenyekevu wa ajabu wa Mtume Mtukufu ﷺ

Kipeenzi chetu Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ, kupitia tabia yake njema ametupa mafunzo mazuri kuhusu kulinda haki za binadamu wenzetu. Hebu tutazame mara moja mfano wa tabia yake njema. Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alitangaza wazi wazi hadharani wakati wa kufa kwake: “Ikiwa natakiwa kumlipa mtu deni lake, ikiwa nimeharibu mali ya mtu au jina, basi natoa maisha, mali na hadhi yangu; jifidieni humu duniani. Musijali ati sitakuwa na raha naye;

haya si maadili yangu. Ikiwa haki ya mtu iko juu yangu ningependa aidha nimpe fidia au anisamehe.” Halafu akasema, “Enyi watu! Mtu ambaye inamjuzu kumregeshea mtu haki yake, amregeshee na asidhani kuwa ataaibika kwani aibu ya humu duniani ni nyepesi mno kuliko ya ahera.” (*Tarikh Dimishq-li-Ibn-e-‘Asākir*, juzuu. 48, uk. 323, *Mulakhkhasan*)

Nimekusongonyoa sikio

Sayyidinā ‘Uṣmān al-Ghanī رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ alimwambia mmoja wa watumwa wake, “Nilikusongonyoa sikio lako kwa hivyo jilipizie kisasi kwangu.” (*Al-Riyāḍ Al-Naḍarāh fī Manāqib Al-Asharāh*, Juz 3, uk. 45)

Muislamu ni nani?

Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema, “Muislamu kamili ni yule ambaye waislamu wengine wamehifadhika na ulimi na mikono yake na muhajiri (mwenye kugura) kamili ni yule ambaye amegura kile kilichokatazwa na Allah عَزَّوَجَلَّ. (*Ṣaḥīḥ Bukhārī*, juzuu. 1, uk. 15, *Ḥadithi 10*)

Kuhusu hadithi hii, mfasiri maarufu wa Qur’an, Muftī Aḥmad Yār Khān عَلَيْهِ رَحْمَةُ الرَّحْمَنِ amesema, “Muislamu kamili ni yule ambaye ni muislamu kwa mtazamo wote; kisharia na kilugha. Muumini kamili ni yule ambaye hasengenyi muislamu, hatukani, hasuti, hapigi mtu na haandiki kukashifu muislamu.” Akaongezea: “Muhajiri kamili ni yule ambaye pamoja na kugura kwao, anagura dhambi.” (*Mirāt-ul-Manājīh*, juzuu. 1, uk. 29)

Kupiga Muislamu jicho na kumtisha

Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema, “Hairuhusiwi kwa muislamu kumtazama muislamu mwenzake kwa namna ambayo ataudhika.” (*Ittaḥaf-ul-Sadat liz Zubaydī, juz. 7, uk. 177*)

Mahali kwengine صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema, “Hairuhusiwi muislamu kumtisha muislamu mwenzake.” (*Sunan Abī Dāwūd, juz. 4, uk. 391, Ḥadithi 5004*)

Ndugu waislamu! Tumekuja kujua kuwa muislamu huwalinda na huwatakia mema waislamu wengine. Kugombana si desturi ya muislamu; husababisha matatizo makubwa, kama alivoeleza Sayyidunā Sheikh Muhammad bin Ismā’il رَحْمَةُ اللهِ الْبَارِي عَلَيْهِ katika mkusanyiko wa hadithi zake, ‘*Ṣaḥīḥ Bukhārī*’. Sayyidinā ‘Ubādāḥ bin Šāmit رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ amesema: Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alitoka kutueleza kuhusu usiku wa Laīla-tul-Qadar; waislamu wawili walikuwa wakigombana. Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akasema, “Nimekuja kuwajulisha kuhusu usiku wa *Laīla-tul-Qadar* kuwa fulani na fulani walikuwa wakigombana, kwa hivyo, ikafutwa (*Laīla-tul-Qadari*) kudhihirishwa kwake.” (*Ṣaḥīḥ Bukhārī, juzuu. 1, uk. 662, Ḥadithi 2023*)

Tuwapole kwa wapole na...

Ndugu waislamu! Kuna mafunzo muhimu katika hadithi hiyo iliyotajwa hapo juu. Kipenzi chetu Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alikuwa tayari kuudhihirisha usiku wa *Laīla-tul-Qadar* lakini

ugomvi baina ya waislamu wawili ulimzuia kufanya hivyo na imebakia ni siri milele. Chukua huu kama mfano, na utafakari ni ubaya ulioje kugombana baina yetu. Lakini nani awezaye kuwafanya watu washindani na wagomvi kuelewa jambo hili? Siku hizi baadhi ya waislamu husema kwa majivuno, “Mtu hawezi kuishi duniani kwa kuwa mpole, tuwe wapole kwa wapole na wahuni kwa wahuni. Na hawesemi tu, bali wanayathibitisha hayo. Wakati mwengine ugomvi hutokea kwa ajili ya jambo dogo na kuzusha vita vya visu na bastola. Yasikitisha kuwa waislamu siku hizi licha ya kuwa waislamu, huuana wao kwa wao, huchoma maduka, magari na mali ya watu na hudai kuwakilisha kabila fulani. Enyi Waislamu! Nyinyi mulikuwa ni walinzi wa kila mmoja wenu, kulikoni? Kipenzi chetu Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema, “Mfano wa waumini katika undugu wa imani, ukarimu, na huruma; ni mfano wa mwili mmoja, kiungo kimoja kikiumizwa, mwili mzima husikia maumivu.” (*Sahīh Muslim, uk. 1396, Hadithi 2586*)

Hata dhalimu usimdhulumu

Imeelezwa katika *‘Tirmizī Sharīf’* kwamba Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema, “Enyi watu Musiwe waigaji, kwa kusema, “ikiwa watu watatufanyia mazuri, tutawafanyia mazuri na wakitufanyia maovu, tutawafanyia maovu.” Lakini jizoesheni tabia ya kwamba ikiwa watu watawafanyia mazuri, pia nyinyi wafanyieni mazuri na wakiwafanyia maovu musiwafanyie maovu.” (*Sunan-ul-Tirmizī, juzuu. 3, uk. 405, Hadithi 2014*)

Safari ya kurudisha kalamu ya mwenyewe

Ndugu waislamu! Mumetanabahi namna gani Maua ya Madani kuhusu tabia ya ukarimu ya kuamiliiana na waislamu ilivyofundishwa na Mtume wetu Mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَسَلَّمَ. Wazee wetu رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى wamekuwa waangalifu kuhusu haki za binadamu na makini katika kuzitekeleza. Sayyidinā ‘Abdullāh bin Mubārak رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى alikaa Syria kwa siku kadhaa. Alikuwa akiandika hadithi. Siku moja kalamu yake ikagoma kuandika, akamuomba mtu kalamu na akasahau kumregeshea na akaichukua nyumbani kwake. Alipokumbuka kuwa ana kalamu ambayo si yake, Sayyidunā ‘Abdullāh bin Mubārak رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى akafunga safiri tena kuelekea Syria ili aregeshe kalamu ya mwenyewe. (*Taḥkīrāt-ul-Wā’iḏīn*, uk. 243)

Vipi unavaa slipa za mwenyewe bila ruhusa?

Ndugu waislamu! Je mumegundua? شَيْخُنَ اللهُ عَزَّوَجَلَّ, wazee wetu walikuwa wakimcha Allah عَزَّوَجَلَّ kikwelikweli kuhusu vitu vya watu. Lakini yasikitisha siku hizi hatuogopi jambo hili. Kumbuka, wakati huu, kwa makusudi, ni rahisi kuweka kitu cha mwenyewe lakini kumfidia Siku ya Kiama mpaka aridhike, itakuwa ni uchungu. Kwa hivyo tuwe waangalifu kuhusu vitu vya watu. Kitu chochote ambacho si chako kama vile tandiko, taulo, vyombo, vitanda, viti nakadhalika, vistumiwe bila ya ruhusa ya mwenyewe. Ikiwa mumekubaliana, haina haja ya kumuomba tena ruhusa. Kwa mfano, mgeni nyumbani, ni kawaida mwenyeji kumruhusu kutumia vyombo hivyo. Aghlabu utapata msikitini mtu akitumia

viatu vya mwenzake kuendea msalani bila ya idhini yake. Linaonekana ni jambo dogo, lakini fikiria kwa muda! Umevaa viatu vya mwenyewe kuendea chooni; mara mwenyewe aje ili aende zake nyumbani. Atakapovikosa atadhani vimeibwa. Hivyo basi ataenda nyumbani miguu chuma na huzuni. Hata ukiviregesha mahali pake, mwenyewe ameshavipoteza. Nani wakulaumiwa? Bila shaka ni wewe na unaweza kuitwa dhalimu. Lahaula! Itasikitisha iliyoje hali ya madhalimu Siku ya Kiama! Sayyidinā Sheikh ‘Abdul Wahhāb Sha’rānī رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ amesema, “Wakati mwengine, mwenye kudhulumiwa hataridhika hata baada ya kuchukuwa matendo mema yote ya dhalimu kwa sababu ya dhuluma moja aliyomfanyia.” (*Tanbīh-ul-Mughtarīn*, uk. 50)

Ndiyo maana wazee wetu walikuwa waangalifu kuhusu mambo ambayo yalionekana kuwa madogo. Sayyidinā Imām Muhammad bin Muhammad Ghazālī رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ amesema:

Alivyokuwa na tahadhari kwa kuvuta harufu ya manukato

Uturi ulikuwa ukipimwa mbele ya Amīr-ul-Mūminīn Sayyidunā ‘Umar bin ‘Abdul ‘Azīz رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ ili kugawanyiwa waislamu; hapo hapo akaziba pua yake ili ajizuie kuvuta harufu ya manukato yale. Watu walipomuona akifanya hivi, yeye رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ akafafanua, “Kuvuta harufu ya manukato ni kuyatumia.” (Kwa vile manukato yako mbele yangu kwa wingi hivyo basi nayavuta kwa wingi na sitaki nifaidike zaidi nikilinganishwa na waislamu wengine kwa

kuvuta harufu zaidi ya manukato.) (*Ihyā-ul-'Ulūm, juzuu. 2, uk. 121; Qūt-ul-Qulūb, juzuu. 2, uk. 533*) Allah ﷺ amrehemu na atusamehe kwa baraka yake!

آمِينَ بِجَاهِ النَّبِيِّ الْأَمِينِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

Kuzima kandili!

Imeelezwa katika '*Kīmīyā-e-Sa'ādat*' kwamba walii mmoja alikuwa amekaa kando ya kitanda cha mgonjwa. Mgonjwa akafa kwa qadari ya Allah ﷺ. Tazama sifa kubwa ya fikra ya kiMadani ya walii huyu. Aliizima kandili mara moja na akasema, "Sasa warithi wake pia wanahaki ya mafuta ya kandili hii." (*Kīmīyā-e-Sa'ādat, juzuu 1, uk. 347*) Allah ﷺ awarehemu na atusamehe kwa baraka yao!

آمِينَ بِجَاهِ النَّبِيِّ الْأَمِينِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

Bustani la Peponi au Shimo la Motoni

Allah, Allah! Ni fikra njema ya kiMadani iliyoje waliyokuwa nayo mawalii wetu عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْعَمِيمِينَ. Sisi wenyewe hatuwezi hata kudhania hivyo. Aūliyā رَحْمَتُهُ اللَّهُ تَعَالَى walitetemeka kwa hofu ya Allah ﷺ; hawakuwa wasahaulifu kuhusu kufa kwao wala kudharau maswala ya kaburi na Siku ya Kiama. Lahaula! Mambo ambayo mtu atakabiliana nayo kaburini yanatisha. Lo! Tutafikwa na nini! Hatujali kuhusu makaburi yetu. Imeelezwa katika '*Ihyā-ul-'Ulūm*': Sayyidinā Sufyān Šaurī رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَلَيْهِ amesema,

“Mtu anayekumbuka kaburi lake mara kwa mara, atalipata kuwa bustani la Peponi baada ya kifo chake; na ambaye husahau atalipata kuwa ni shimo la Motoni.” (*Iḥyā-ul-'Ulūm, juzuu. 4, uk. 238*)

Tende nusu

Kumbuka! Ni muhimu kuchunga haki za watoto wadogo. Kudharau haki zao kunaweza kukutia Motoni na kuzichunga kunaweza kukutia Peponi. Sayyidinā Muhammad bin Ismā'il Bukhārī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْبَارِي ameeleza katika mkusanyiko wa hadithi zake 'Ṣaḥīḥ Bukhārī': Umm-ul-Mūminīn Sayyidatunā 'Āishah Ṣiddīqah رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهَا amesema, “Mwanamke alikuja kwangu pamoja na wanawe wawili wa kike na akaniomba msaada. Wakati huo nilikuwa na tembe moja tu ya tende, kwa hivyo nikampa yeye. Aliigawanya mara mbili. Akampa kila mtoto nusu moja.” Sayyidatunā 'Āishah Ṣiddīqah رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهَا alipomuelezea Mtume Mtukufu صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ, kisa hiki Alisema صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ, “Aliyebahatika kuwa na watoto wakike na akawalea kwa tabia njema, basi watoto hawa watakuwa kinga ya yeye kuingia Motoni.” (*Ṣaḥīḥ Bukhārī, juzuu. 4, uk. 99, Hadithi 5995*)

Matokeo ya kofi la mfalme

Sayyidunā 'Umar al-Fārūq al-A'ẓam رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهُ hangeweza kumuhurumia yeyote kuhusu haki ya binadamu. Mfalme wa Ghassān hivi karibuni alisilimu. Jambo hili lilimfanya Sayyidunā 'Umar al-Fārūq al-A'ẓam رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهُ kufurahi kwa sababu lilileta matumaini kuwa watu wa milki yake pia wataukubali

uislamu. Wakati wa kutufu al-Kaaba, Bedui maskini, bila kukusudia aliikanyaga nguo ya mfalme. Kwa hasira mfalme alimpiga kofi kwa nguvu iliyosababisha Bedui kung’oka jino. Bedui akadai haki katika mahakama ya Sayyidunā ‘Umar al-Fārūq al-A’zam رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ. Mfalme alipokubali kuwa alimpiga kofi Bedui, Sayyidinā ‘Umar al-Fārūq al-A’zam رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ alimwambia Bedui aliyedhulumiwa kwamba anaweza kumlipiza mfalme wa Ghassān kisasi. Mfalme akabishana, “Vipi mtu wa kawaida anaweza kuwa sawa na mfalme na anahaki ya kulipiza kisasi kutoka kwangu? Sayyidinā ‘Umar رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ akasema, “Uislamu umekufanya wewe na yeye muwe sawa.” Mfalme akaomba ruhusa ya siku moja lakini akatoroka usiku na akaritadi. (*Khuṭbāt-e-Muḥarram, uk. 138*)

Sayyidunā ‘Umar al-Fārūq aliishi maisha ya

Kawaida رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ

Ndugu waislamu! Sayyidinā ‘Umar رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ hakuonesha huruma kwa mfalme wa Ghassān. Mfalme yule kuukataa uislamu na kuwa murtad hakukusababisha madhara yoyote kwa uislamu. Kama Sayyidunā ‘Umar رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ angeonesha huruma, sifa ya uislamu ingekuwa imeharibika. Watu wangepata fikra kwamba مَعَاذَ اللَّهِ عَزَّ وَجَلَّ Uislamu hauwezi kuwalazimisha watu wenye nguvu kulipa haki za wanyonge. Ni kutokana na uadilifu wake huu ambapo siku moja wakati wa kiangazi, Sayyidinā ‘Umar al-Fārūq al-A’zam رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ alikuwa amejituliza chini ya mti akiwa amelalia jiwe na wala hakuwa na mlinzi yeyote; Wakati huo

mjumbe kutoka Roma akamjia. Mjumbe akashangaa kumuona amelala namna ile na akafikiria iwapo huyu ndiye mtu yule yule ambaye huwafanya watu wa ulimwengu mzima kuwa na hofu! Halafu akasema, “Ewe ‘Umar رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ! Wewe wafanya haki na kuchunga haki za binadamu kwa hivyo unapata usingizi mzuri hata juu ya mawe? Ilihali wafalme wetu wanawagandamiza watu, wanakanyaga haki zao, kwa hivyo hawawezi kulala hata katika vitanda vyao vyenye magodoro laini.” Allah عَزَّوَجَلَّ amrehemu na atusamehe kwa baraka yake!

أَمِينٌ بِجَاهِ النَّبِيِّ الْأَمِينِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

Sababu za mwisho mbaya

Hebu tafakari matokeo mabaya ya udhalimu yaliyomfanya mfalme wa Ghassān kupoteza imāni yake! Sayyidinā Abū Bakr Warrāq رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ amesema, “Kudhulumu watu huwa ni sababu ya kupoteza imani.” Mtu mmoja alimuuliza Sayyidinā ‘Abul Qāsīm Ḥakīm رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ, “Kuna dhambi ambayo yaweza kumfanya mtu akapoteza imani yake?” Akajibu, “Kuna sababu tatu za kupoteza imani:

1. Kutomshukuru Allah عَزَّوَجَلَّ kwa neema ya imani
2. Kutoogopa kupoteza imani
3. Kudhulumu muislamu.” (*Tanbīh-ul-Ghāfilīn*, uk. 204)

Je, ni vipi kujiita mtumwa wa mwengine?

Mawalii wetu wameweka mifano mizuri kuhusu kulinda haki za binadamu. Kwa hivyo, Sayyidinā Imām Abū Yūsuf رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ, aliyekuwa Hakimu Mkuu wakati wake na mwanafunzi wa Imām al-A'ẓam Abū Ḥanīfah رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ, alikataa ushahidi wa, Faḍl bin Rabī', Waziri mwaminifu wa, Khalifa Ḥārūn-ur-Rashīd عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللهِ التَّجِيد. Khalīfah Ḥārūn-ur-Rashīd alipotaka kujua sababu ya kukataa kwake, alijibu; “Siku moja nilimsikia mwenyewe akikwambia, “Mimi ni mtumwa wako”, ikiwa kauli yake ni ya kweli, basi hafai kutoa ushahidi kwa ajili yako kwa sababu ushahidi wa mtumwa kwa bwana wake haukubaliki. Na ikiwa alisema uongo ili kukusifu tu, hata hivyo pia ushahidi wake haukubaliwi kwani anayeweza kusema uongo wazi wazi mbele ya mahakama yako atashindwa vipi kutoa ushahidi wa uongo katika mahakama yangu!”

Wasikiaje?

Ndugu waislamu! Je, mumegundua? Sayyidinā Imām Abū Yūsuf رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ alikuwa na akili na mwangalifu mno na muadilifu katika mambo yanayohusu sharia na hakusita kuukataa ushahidi wa waziri wa Khalifa. Ni vyema kuzingatia kuwa wakati mwengine, bila kujua au kwa ajili ya kufurahisha mtu, mtu hujiita mtumwa wa mwengine; lakini moyoni ni kinyume. Mungu azijaaliye nyoyo na ndimi zetu zinyoke! Mawalii wetu walikuwa waangalifu mno kuhusu jambo hili na walisema kile ambacho walikusudia. Sayyidinā Imām Muhammad Ibn Sīrīn عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللهِ التَّجِيد alimuuliza

mtu “Wasikiaje?” Akajibu, “Mtu atasikia vipi ikiwa anadaiwa Dirham 500/= na anajukumu la nyumbani katika hali ambayo hana hata dirham moja.” Sayyidinā Imām Muhammad رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ alimletea Dirham 1,000/= kutoka nyumbani kwake. Akamwambia, “Lipa deni lako la Dirham 500/= na zibakiazozuweke kwa ajili ya matumizi ya nyumbani.” Baada ya kisa hicho, Sayyidinā Imām Muhammad رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ aliamua kutomuuliza mtu yeyote hali yake siku zijazo. Sayyidinā Imām Muhammad bin Muhammad Ghazālī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللهِ الْوَالِي amesema: Imām Ibn Sīrīn عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللهِ الْفَيْدِين aliamua kutomuuliza mtu hali yake kwa sababu alikuwa na mtazamo, “iwapo nitamuuliza mtu hali yake na mtu huyo aniambiye shida zake, na nisimsaidiye basi nitaonekana ni ‘mnafikī’.” (*Kimīyā-e-Sa’adat, juz. 1, uk. 408*)

Ufafanuzi wa ‘Nitaonekana mnafikī’

Ndugu waislamu! Je mumetanabahi? Mawalii walikuwa waongofu na wakweli. Waliamini kwamba mtu asimuulize mtu hali yake ila tu ikiwa anamuhurumia kikweli kweli. Na ikiwa utamuuliza hali yake, na akwambie shida zake; basi umsaidie kiasi unachoweza. Kumbuka! Maneno ya Imām Ibn Sīrīn عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللهِ الْفَيْدِين “Nitaonekana mnafikī’ ikiwa sitaweza kumsaidia”, yana maana kuwa mnafikī wa vitendo wala si wa imani.

Ni muhimu kumsaidia madhulumu

Kudhulumu watu ni kwenda kinyume na haki za binadamu, na ni hatia kutosaidia aliyedhulumiwa ilihali una uwezo. Sayyidinā

‘Abdullāh Ibn-e-‘Abbās رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُمَا ameeleza kwamba Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema, “Allah عَزَّوَجَلَّ amesema: Naapa kwa heshima na utukufu wangu hakika, nitamlipiza kisasi dhalimu mapema au baadaye. Na nitamlipiza yule ambaye hasaidii wadhulumiwa ingawa ana uwezo wa kufanya hivyo.”

(Attarghīb Wattarhīb, juz. 3, uk. 145, Hadithi 3421)

Hivyo basi tumetanabahi kuwa ambaye hasaidii anayedhulumiwa ilihali ana uwezo wa kumsaidia ni mtenda dhambi. Lakini yule ambaye hana uwezo wa kumsaidiya hana dhambi kama alivyosema Mufti Muhammad Sharīf-ul-Ḥaq Amjadī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللهِ الْقَوِي, “Kumbuka! Kumsaidia muislamu wakati mwengine ni faradhi au wajibu au mustahabu. Inategemea hali ya anayesaidia.

(Nuzḥat-ul-Qārī, juz. 3, uk. 665)

Miale ya moto ilikuwa inatoka kaburini

‘Allāmah Abū Yūsuf Muhammad Sharīf Kotalvī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللهِ الْقَوِي ameeleza katika kitabu chake ‘*Akhlāq-us-Ṣāliḥīn*’, Abū Maīsarāh عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى amesema: Maiti alikuwa akiadhibiwa na miale ya moto ilikuwa inatoka kaburini. Maiti akawauliza malaika, “Kwa nini munanipiga?” Malaika wakajibu, “Siku moja madhulumu alikuomba msaada lakini hukumsaidia na mara moja ulisali bila udhu.” *(Akhlāq-us-Ṣāliḥīn, uk. 57; Tanbīh-ul-Mughtarīn, uk. 51)*

Huruma kwa waislamu

Ndugu waislamu! Haya yalikuwa ni kuhusu yule ambaye ana uwezo wa kuwasaidia madhulumu lakini hakuwasaidia. Je,

itakuwaje hali ya madhalimu! Na tumepata kujua kuwa tunatakiwa kusaidia madhulumu kwani kufanya hivyo kuna thawabu kubwa. Jaribu kutafakari mawalii wetu walivyokuwa na wasiwasi juu ya masaibu ya waislamu kiasi gani. Zingatia kisa kilichotajwa katika *‘Kīmīyā-e-Sa’ādat’* ya kwamba siku moja watu walimuona Sayyidunā Fuḍayl bin ‘Ayāz رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَلَيْهِ akilia. Walipouliza sababu, alijibu, “Nalia kwa ajili ya wale waislamu walionidhulumu ya kwamba Siku ya Kiama watakapoulizwa sababu ya kufanya hivyo; hawatosikilizwa na watafedheshwa na kuaibishwa.” (*Kīmīyā-e-Sa’ādat, juz. 1, uk. 393*)

Huruma kwa mwizi

Mtu mmoja alimwibia Mcha Mungu pesa. Mcha Mungu akaanza kulia. Watu walipomuhurumia, alisema, “Sililii pesa zangu bali namlilia mwizi kwa kuwa atahukumiwa Siku ya Kiama na wakati huo atafedheheka kiasi gani!”

Adhabu ya ujambazi

Hebu niwaeleze adhabu ya ujambazi. ‘Abul Laiš Samarqandī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى ameeleza katika *‘Qurrā-tul-‘Uyūn’*: Ambaye amemuibia mwenziwe hata kiasi kidogo cha pesa kitatundikwa shingoni mwake kama mkufu Siku ya Kiama. Na aliyekula kutokana na mapato ya haramu kidogo, moto utawashwa tumboni mwake na atapiga ukemi wa kutisha ajabu hata wale wanaofufuka kutoka makaburi yao watatetema, mpaka atakapohukumiwa mbele ya Allah عَزَّوَجَلَّ.” (*Qurrā-tul-‘Uyūn, uk. 392*)

Mau ya Madani kwa wale wanaowatibu waovu

Ndugu waislamu! Mada inayojadiliwa ilikuwa ibakize huruma kwa waislamu. Mawalii wetu walionesha huruma kwa waislamu. Wakizingatia adhabu ambayo watu wangepata kwa kutenda dhambi, mawalii wetu waliwahurumia na walijitahidi kuwarekebisha. Nasi pia tujitahidi na tuwe na moyo kuwarekebisha kwa kutumia busara. Mbinu anazotumia daktari kwa mgonjwa zinaweza kuwa na mafunzo kwetu. Daktari hamchukii mgonjwa hata kama anamkaidi kwa ajili ya uchungu wa sindano au dawa chungu. Hata hivyo daktari humshughulikia mgonjwa kwa njia ya upole. Kwa hivyo mgonjwa anayeugua dhambi akitufanyia kejeli au kutuchukulia vibaya, tusivunjike moyo; bali tuendelee kumtibu. Ikiwa tutaendelea kumshawishi kusafiri katika Madanī Qafilāh, basi **إِنَّ شَاءَ اللَّهُ عَزَّوَجَلَّ**. Kwa uwezo wa Allah **عَزَّوَجَلَّ** atapona.”

Mbinu za kujifunza haki za wengine

Kumbuka! Miongoni mwa haki za binadamu wenzako, ya kwanza kabisa ni haki ya wazazi. Kujifunza haki zao, sikiliza bayana kutoka CD *‘Mā Bāp ko Satānā Ḥarām ḥay’* (Ni haramu kuwaudhi wazazi) ilyotolewa na Maktaba-tul-Madīnah na VCD ya *‘Mā Bāp kay Ḥuqūq’* (Haki za wazazi wawili) ya Nigrān-e-Shūrā. Vile vile haki za watoto, mume, mke, jamaa, jirani na kadhalika pia zina umuhimu. Si rahisi kujifunza haki zote hizi katika bayana fupi kama hii; kwa hivyo pitia vitabu vitatu vifuatavyo vilivyochapishwa na Maktaba-tul-Madīnah:

1. Wālidāin, Zaujaīn aur Asātīzah kay Ḥuqūq (Haki za wazazi, mume na mke na walimu)
2. Ḥuqūq-ul-‘Ibād kaysay Mu’āf ḥaun (Haki za binadamu zitasamehewa vipi)
3. Awlād kay Ḥuqūq (Haki za watoto)

Pia endelea kusafiri katika Madanī Qāfilah. Pamoja na kujua haki za binadamu **إِنْ شَاءَ اللَّهُ عَزَّوَجَلَّ**, itasababisha pia kuwa na moyo wa kuwa mwangalifu. Na tukiwa waangalifu **إِنْ شَاءَ اللَّهُ**, njia ya kwenda Peponi inakuwa nyepesi.

Namna mbalimbali za kudhulumu

Wale wanaowavunjia heshima waislamu, wanaowaudhi, wanaotamka majina yao vibaya, kuwaharibia majina kuwakosoa na kuwadhihaki; ni sharti wamuogope Allah **عَزَّوَجَلَّ**. Sikizeni! Allah **عَزَّوَجَلَّ** ameeleza katika Sūrah Al-Ḥujurāt, juzuu 26, aya 11:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا يَسْخَرْ قَوْمٌ مِّنْ قَوْمٍ عَسَىٰ أَن يَكُونُوا
خَيْرًا مِّنْهُمْ وَلَا نِسَاءٌ مِّنْ نِّسَاءٍ عَسَىٰ أَن يَكُنَّ خَيْرًا مِّنْهُنَّ
وَلَا تَلْبِسُوا أَنفُسَكُمْ وَلَا تَنَابَرُوا بِاللِّقَابِ ۗ بئسَ الإِسْمُ الفُسُوقُ
بَعْدَ الإِيمَانِ ۗ وَمَنْ لَّمْ يَتُبْ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿١١﴾

Enyi mulioamini! Wanaume wasiwadharau wanaume wenzao wala wanawake wasiwadharau wanawake wenzao; huenda hao wakawa bora kuliko wao. Wala musivunjiane heshima. Wala musiitane kwa majina ya kejeli. Ni uovu kutumia jina baya baada ya kwisha amini. Na wasiotubu, hao ndiwo wenye kudhulumu.

[Kanz-ul-Īmān (Translation of Quran)] (Sūra 26, Sūrah Hujurāt, Aya 11)

Ni dhambi kumfanyia mtu mzaha

Ndugu waislamu! Ni dhambi kucheka umaskini wa mtu, asili au kasoro ya maumbile yake au pia kumbandika mtu jina ambalo jamii inalichukulia kuwa ni baya. Hatuwezi kumuita mtu ‘mbwa’ au ‘punda’ au ‘nguruwe’ na kadhalika. Vile vile hatuwezi kumuita mtu mwenye kasoro ya kimaumbile kwa kasoro hiyo. Kwa mfano, kipofu, mlingoti na kadhalika. Lakini inaruhusiwa kumrejelea kwa kasoro yake ikiwa lengo ni kumtambua pale inapojuzu. Qur’ani Tukufu imewatangaza kuwa mafasiki wanaowacheka watu, kuwabandika majina ambayo jamii inayachukulia kuwa siyo mazuri na kuwafanyia mzaha. Wale ambao hawatubu kwa tendo hili baya wametangazwa kuwa madhalimu na Qur’an Tukufu. Enyi munaowakejeli wengine, sikilzeni kwa makini!

Adhabu kwa kukejeli wengine

Kila unapotaka kuwakejeli wengine, kwanza zingatia maneno Mtume Mtukufu ﷺ: “Siku ya Kiama, mtu aliyekuwa na tabia ya kuwakejeli wengine, mlango wa Peponi utafunguliwa

halafu ataitwa. Ataelekea huko kwa hamu. Atakapoukaribia mlango, mlango utafungwa. Mlango mwengine wa Peponi utafunguliwa tena na ataitwa ili aingie. Ataelekea huko kwa hamu lakini atakapoukaribia mlango huo vile vile utafungwa. Ataendelea hivyo mpaka utakapofunguliwa tena mlango atakataa kuingia.” (*Kitāb-us-Şamt ma’ Mawsū’ah’ Imām Ibn-e-‘Abī Dunyā, juz. 7, uk. 183-184, Hadithi 287*)

Tafadhali omba msamaha

Ndugu waislamu! Muogopeni Allah عَزَّوَجَلَّ na ombeni msamaha. Katika kuvunja haki ya binadamu, haitoshi kumuomba msamaha Allah عَزَّوَجَلَّ; haki zilizovunjwa ni lazima zilipwe. Kwa mfano, ikiwa haki ya pesa imevunjwa, pesa lazima zilipwe pia; ikiwa mtu aliudhiwa, dhalimu lazima amuombe msamaha aliyemdhulumu. Omba msamaha kwa wote wale ambao uliwakejeli, uliowaita kwa majina mabaya, uliowachafulia majina yao na kuwadhihaki, kumtizama mtu mpaka akaudhika, kumtisha, kumtukana, kumpiga, kutomuheshimu au kumsengenyana akajua. Kwa jumla ikiwa umesababisha maudhi kwa namna yoyote waombe wote msamaha. Ikiwa utajizuiwa kuomba msamaha ukizingatia kuwa kuvunja hadhi yako, basi fikiria! Kutatokea nini ikiwa watachukua amali yako njema na wewe upewe madhambi yao Siku ya Kiama! Naapa kwa jina la Allah عَزَّوَجَلَّ hadhi yako kwa hakika itapotea wakati huo na hakuna rafiki, ndugu wala jamaa atakayekuwapo kukusaidia. Tafadhali fanya haraka! Waangukie wazazi wako, waombe msamaha jamaa zako,

waangukie wafanyikazi wako, patana na ndugu na marafiki zako waislamu; kwa kujidhalilisha mbele yao na kuomba msamaha leo ulimwenguni ili ufaulu kupata heshima ya ahera. Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَسَلَّمَ amesema, 'مَنْ تَوَاصَعَ لِلَّهِ رَفَعَهُ اللَّهُ': "Mwenye kunyenyekea kwa ajili ya Allah عَزَّوَجَلَّ, Allah عَزَّوَجَلَّ humtunuka utukufu."

(Shu'ab-ul-Īmān, juz. 6, uk 297, Ḥadīthi 8229)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Nimeshamsamehe

Watu wengi wanauhusiano na mimi na kwa yule ambaye ana uhusiano na watu wengi, kuna nafasi kubwa ya kuvunja haki za wenzake. Lo! Sijui itakuwa nimewaudhi wangapi! Huenda ikawa nimewaudhi watu kadhaa! Nawaomba nyote kwa unyenyekevu ikiwa nimemuudhi mtu kimwili, kifedha au hadhi yake; ima alipize kisasi au anisamehe. Ikiwa natakiwa kulipa deni la mtu, aje nimlipe, na ikiwa hataki nimlipe, namuomba anisamehe. Ama kwa ninaowadai ninawasamehe. Ewe Allah عَزَّوَجَلَّ, tafadhali usimuadhibu muislamu yeyote kwa ajili yangu. Ninamsamehe kila muislamu katika haki zangu; ikiwa mtu aliniudhi, alinipiga au atanipiga, au alijaribu kuniua au atajaribu au hata yule ambaye atafaulu kuniua. Nathibitisha kwamba ninawasamehe waislamu wote katika haki zangu. Ewe Allah عَزَّوَجَلَّ! Mimi ni mja wako dhaidu, maskini nisamehe madhambi yangu yote yaliyopita na yatakayokuja bila ya hesabu ya matendo yangu.

Ndugu wote waislamu ambao wamehudhuria Ijtimai hii ya kimataifa ya siku tatu, au wanatazama katika Idhaa ya Madani au kupitia mtandao au wananisikiliza kupitia CD au wanasoma bayana hii iliyochapishwa; tafadhali kuweni wasikivu. Haki ambayo inatambulikana kuwa kubwa kushinda zote, chukuliya kwamba nimekuvunjia haki hiyo na kama kuna zingine ambazo nimekuvunjia basi kwa ajili ya Allah **عَزَّوَجَلَّ**, nisamehe. Pia nakuomba unisamehe haki zako ambazo huenda nikazivunja siku zijazo. Tafadhali, sema kwa dhati ya moyo wako, “Nimekusamehe.” **جَزَاكُمُ اللَّهُ خَيْرًا وَأَحْسَنَ الْجَزَاءِ**

Pesa zirudishwe

Anayedaiwa lazima alipe na pia aombe msamaha iwapo amelichelewesha. Kwa wale wote ambao walikuhonga, au kuwanyang'anya kwa mabavu inafaa uwaregeshee vitu vyao au uwaombe wakupe muda ili uwalipe au wakusamehe kwa kila unachofaa kuwalipa au kuwaregeshea. Pia omba msamaha kwa usumbufu ambao huenda uliwasababishia. Ikiwa mtu huyo amekufa, basi warithi wake waandamwe na walipwe. Ikiwa hakuna warithi, basi toa kiwango sawa kwa sadaka. Ikiwa mtu alinyakua mali ya watu lakini hawakumbuki wenyewe, hata yeye basi pia atoe kiwango sawa kama sadaka yaani awape masikini. Ikiwa mdhulumiwa atadai haki yake hata baada ya yeye kuitoa mali kama sadaka, vile vile anawajibika kumlipa.

Namna ya kuomba msamaha wale tuliowasahau

Kwa wale ndugu waislamu ambao humcha Allah ﷺ kuhusu mambo ya haki za binadamu na wamechanganyikiwa kuwa huenda ikawa wamevunja haki za watu kadhaa na kuwaudhi; watampata vipi kila aliyedhulumika! Kwa hivyo wale ambao uliwaudhi na unaweza kuwapata, kutana nao au wasiliana nao ima kupitia simu au barua na kwa njia yoyote jaribu kuwashawishi wa kusamehe. Na kwa wale ambao wamepotea au kufa au huwakumbuki uliwaudhi, basi waombe dua kwa Allah ﷺ. Kwa mfano fanya desturi ya kuomba hivi kila baada ya sala: “Ewe Allah ﷺ! Nisamehe na waislamu wote ambao haki zao nimezivunja mpaka leo.” Usivunjike moyo kwa sababu rehema za Allah ﷺ hazina kikomo. وَإِنْ شَاءَ اللَّهُ ﷺ majuto yako ya dhati yatazaa matunda na kwa baraka ya Mtume ﷺ, Mwenye Rehema, Allah ﷺ atakuchukulia kwa huruma kwa kukupa nafasi zitakazokuongoza kupata msamaha wa kuvunja haki za binadamu.

Allah ﷺ atapanga kupatana

Sayyidunā Anas رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهُ amesema: Siku moja alikuwapo Mtume Mtukufu ﷺ, Yeye ﷺ akatabasamu. Sayyidinā ‘Umar al-Fārūq رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهُ akauliza, “Ewe Rasūlallāh ﷺ! Wazazi wangu watolewe sadak kwa ajili yako wewe; kwa nini ukatabasamu?” Mtume Mtukufu ﷺ akajibu, “Watu wawili katika umma wangu watainama kwa heshima katika mahakama ya Allah ﷺ,

mmoja atashtaki, “Ewe Allah **عَزَّوَجَلَّ**! Nipe haki, amenidhulumu.” Allah **عَزَّوَجَلَّ** atamwambia mlalamishi “Sasa huyu mtu maskini (mshtakiwa) afanye nini, hana amali njema alizobakishwa nazo.” Mlalamishi atasema, “Zigurishe dhambi zangu kwake.” Mtume Mtukufu **صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ** akaanza kulia baada ya kusema hayo na akasema: Siku hiyo ni siku nzito sana kwa sababu kila mmoja atakuwa katika hali ya kutaka kupunguza mzigo wake. Allah **عَزَّوَجَلَّ** atamwambia mlalamishi, “Angalia vilivyoko mbele yako!” Atajibu, “Ewe Mwenyezi Mungu! Naweza kuona miji mikubwa na makasri ya dhahabu yaliyopambwa kwa lulu. Miji hii na majumba haya mazuri ni ya Mtume au muumini au shahidi gani?” Allah **عَزَّوَجَلَّ** atajibu, “Haya ni ya wale ambao watalipa malipo yake na wayanunue.” Mlalamishi atauliza, “Kina nani hao ambao wanaweza kulipa malipo yake?” Allah **عَزَّوَجَلَّ** atajibu, “Wewe Unaweza.” Atauliza, “Kivipi?” Allah **عَزَّوَجَلَّ** atamjibu, “Kwa kumsamehe nduguyo kwa haki aliyoivunja.” Mlalamishi atasema, “Ewe Allah **عَزَّوَجَلَّ**! Nimesamehe haki zangu zote.” Allah **عَزَّوَجَلَّ** atasema, “Shika mkono wa ndugu yako na ingieni Peponi pamoja.” Halafu Mtume Mtukufu **صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ** akasema, “Muogope Allah **عَزَّوَجَلَّ** na upatanishe miongoni mwa watu kwa sababu Siku ya Kiama, Allah **عَزَّوَجَلَّ** atapanga kuwapatanisha miongoni mwa waislamu.” (*Al-Mustadrak-lil-Hākim, juz. 5, uk. 795, Hadithi 8758*)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Ndugu waislamu! Nikihitimisha bayana yangu, ningependa kuwapa faida ya kuwaelezea uzuri wa suna na baadhi ya matendo

na tabia za suna. Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema, “Anayependa suna zangu, amenipenda mimi na anayenipenda, atakuwa pamoja nami Peponi.” (*Mishkāt-ul-Maṣābīh*, juz. 1, uk. 55, *Hadithi 175*)

Maua 12 ya Madani yanayohusu mazungumzo

Zungumza kwa tabasamu na uso mkunjufu.

1. Kwa nia ya kuridhisha waislamu, heshimu wakubwa na kuwa na tabia ya ukarimu kwa wadogo. إِنَّ شَاءَ اللهُ عَزَّوَجَلَّ, mbali na kupata thawabu, utabakia kuheshimiwa mbele ya macho ya wao wote.
2. Si sunna kupaaza sauti (jambo ambalo limekuwa kawaida miongoni mwa marafiki siku hizi) wakati wa mazungumzo miongoni mwa marafiki. Hata kwa motto mchanga aliyezaliwa leo, zungumza naye kwa heshima na nia njema. إِنَّ شَاءَ اللهُ عَزَّوَجَلَّ, itaimarisha nidhamu yako na mtoto atajifunza tabia njema.
3. Si vizuri kugusa sehemu za siri, kutoa uchafu mwilini kwa kutumia vidole, kugusa pua mara kwa mara mbele ya watu wengine au kutia kidole katika pua au sikio au kuendelea kutema mate kwani watu wanachukia matendo kama hayo.
4. Mtu anapozungumza msikilize kwa makini mpaka amalize. Ukimkatiza wakati anapozungumza ni kinyume na sunna.

5. Usicheke kwa nguvu/ kwa sauti kwani Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ hakucheka kwa nguvu maishani mwake.
6. Kuzungumza kupita kiasi na kucheka kwa sauti kunakuharibia hadhi yako.
7. Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema, “Ukimuona mtu ameipa nyongo dunia na ana tabia ya kutozungumza sana, basi kuwa karibu naye na uwe pamoja naye kwani amebarikiwa na hekima.” (*Sunan Ibn-e-Mājah*, juzuu. 4, uk. 422, *Hadithi 4101*)
8. Amesema Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ, “Aliyenyamaza amepata uokozi.” (*Sunan Tirmizi*, juzuu. 4, uk. 225, *Hadithi 2509*)
9. Imetajwa katika Mirāt-ul-Manājih: Sayyidina Imām Ghazālī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللهِ الْوَالِي amesema, “Kuna aina nne za mazungumzo: (i) yenye madhara matupu (ii) yenye faida tupu (iii) yenye madhara na faida na (iv) yasiyokuwa na faida wala madhara. Daima yafaa kuepuka mazungumzo yenye madhara matupu na kuzungumza mazungumzo yenye faida tupu. Ni bora kuepuka mazungumzo yenye faida na pia madhara na kujihusisha na mazungumzo yasiyo na faida wala madhara ni kupoteza wakati. Ni vyema unyamaze kwa sababu ni vigumu kutofautisha kati ya mazungumzo haya.” (*Mirāt-ul-Manājih*, juz. 6, uk. 464)
10. Lazima kuwe na lengo katika kila mazungumzo na zingatia mawazo na hali ya wasikilizaji unapozungumza.

11. Daima epuka mazungumzo yasiyokuwa na heshima na makali, lugha chafu na usitukane mtu. Kumbuka! Ni haramu kabisa kwa mujibu wa sharia kumtukana muislamu. (*Fatāwā-e-Razawiyah, juz. 21, uk. 127*)
12. Pepo imeharamishwa kwa mtu ambaye huzungumza maneno machafu. Mtume Kipenzi صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema, “Imeharamishwa pepo kwa mtu ambaye huzungumza maneno machafu.” (*Kitāb-us-Şamt ma’ Mawsū’ah Al-Imām Ibn-e-Abī al-Dunyā, juz. 7, uk. 204, Raqam 325*)

Tafadhali pitia kitabu “*Sunnatayn aur Ādāb*”, (Sunna na adabu) kilicho na kurasa 120, kilichochapishwa na Maktaba-tul-Madīnaḥ ili upate maelezo zaidi kuhusu adabu ya mazungumzo kwa mujibu wa maadili ya kiislamu na ujifunze suna zaidi za Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ. Kusafiri pamoja na kundi la Madanī Qafilah pamoja na wapenzi wa Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ ni njia moja wapo bora ya kujifunza na kufuata suna za Mtume Kipenzi صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ